

PAMBANO KUU

Pambano Kuu: Chanzo cha Uovu na Ushindi wa Mungu

Kwa nini kuna dhambi, maumivu na mateso kama Mungu ni mwema? Somo hili la Imani ya Msingi Na. 8 linachunguza chanzo cha Pambano Kuu, wahusika wake, mbinu za Shetani na...

PR. ALMODAD AMOS YARAGWILLER

2026

Muhtasari

Hili ni somo moja miongoni mwa masomo Manne yanayoangukia katika kundi la Mafundisho ya Biblia linaloitwa Fundisho Kuhusu Wokovu. Somo hili linaitwa Pambano Kuu, ambalo ni Imani ya Msingi No. 8 miongoni mwa Imani za Msingi 28 kama zinavyofundishwa na Kanisa la Waadventista wa Sabato. Baadhi ya mambo tutakayoangazia katika somo hili li pamoja na:

- Maana ya Pambano Kuu
- Eneo pambano hili linapofanyikia
- Mwasisi wa pambano hili
- Wahusika wakuu wa pambano hili
- Mbinu zinazotumika katika Pambano
- Na hatimaye mpango wa Mungu katika Pambano Hili.

Utangulizi

Huhitaji kuchagua ili uingie ndani ya hili pambano. Tayari wote tumeshahusishwa. Na hata maisha ambayo tunaishi yamekaa mkao wa Pambano: Kuna mbele na nyuma, kuna kulia na kushoto, kuna kupata na kupoteza, kuna furaha na huzuni, n.k. Ukiichunguza Biblia kwa umakini utaona sura mbili zinazojitokeza toka mwanzo wa Biblia mpaka mwisho wake: Angalia mifano hii michache:

- Kuna kweli na uongo
- Kuna watoto wa Mungu na kuna watoto wa Ibilisi
- Kuna uzima wa milele na kuna mauti ya milele

- Kuna upande wa nuru na kuna upande wa giza
- Kuna mlango mwembamba na kuna lango pana
- Kuna njia nyembamba na kuna njia pana
- Kuna mpanzi wa mbegu njema na mpanzi wa magugu
- Kuna kundi la kondoo na kunzi la mbuzi

Mwonekano wa Athari za Pambano

Wanadamu wengi wameelekeza fikra zao katika kutafuta chanzo na sababu hasa ya kuwepo kwa pande hizi mbili ambazo zimezaa taabu na mahangaiko makubwa katika ulimwengu huu. Mwisho wa tafiti zote huwa wanadamu wanagundua kwamba uovu ndicho chanzo cha matatizo yote yanayomkabili mwanadamu. Wanadamu Wameona madhara ya uovu, na matokeo yake ya kutisha, na sasa swali kubwa wanalojihoji ni kwamba yawezaje yote haya kutokea chini ya utawala wake Yeye aliye Mtakatifu, tena aliye na uwezo na upendo mwingi? Maswali mengine yanayoambatana na hoja hii ya msingi ni kama vile:

- Kwa nini kuna dhambi, maumivu na mateso?
- Ikiwa Mungu ni mwema kwa nini dunia inaonekana mbaya kiasi hiki?

Kwa nini Mungu hakuzuia dhambi isitokee kwa uwezo wake na akaiacha? Hapa kuna fumbo kubwa ambalo wengi wetu hawajapata majibu bado, lakini somo hili litatoa majibu hayo kwa kadri ya nuru iliyofunuliwa kwetu katika maandiko matakatifu.